

Imba Wimbo Kuhusu Ujasiri

Soma Zaburi 27:6. Daudi alipenda muziki, na mara kwa mara aliimba nyimbo za kumsifu Yehova. Nyimbo hizo zilimsaidia kuwa jasiri. Kuimba kunaweza kukusaidia kupata ujasiri pia!

Soma maneno ya wimbo “Tupe Ujasiri.” Wimbo huo unatupa sababu zipi za kuwa na ujasiri? Kariri wimbo huo, na kisha ufanye mazoezi ya kuuimba pamoja na familia yako.

KUNJA



WIMBO 137

Tupe Ujasiri

(Matendo 4:29)

1. Tuhubiripo Ufalme,
Na jina kutangaza,
Ni wengi wanatupinga
Na kutuaibisha.
Hatuogopi watu,
Ni wewe tunayetii.
Twasali tupe roho yako;
Yehova, tusikilize.

(KORASI)

Tupe ujasiri Baba;
Ili tushinde woga.
Tupe uhodari Baba
Tuweze kuhubiri.
Har-magedoni karibu,
Lakini kabla ifike,
Tupe ujasiri Baba.
Twakuomba.

2. Kumbuka sisi mavumbi,
Basi twaogopeshwa.
Tunaamini ahadi
Utatusaidia.
Angalia vitisho
Vya wanaotunyanyasa.
Tupe sote uvumilivu
Tuseme kwa ujasiri.

(KORASI)